HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. ELSIE SIA KANZA, BALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE MKUTANO ALIOUFANYA NA VIONGOZI WA JUMUIYA ZA WATANZANIA NCHINI MAREKANI NA MEXICO

TAREHE 20 JANUARI 2024

Ndugu Viongozi wa Jumuiya za Watanzania;

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi Iendelee!

Nawatakia Nyote Heri ya Mwaka Mpya 2024!

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutupa uhai na kutuwezesha kukutana leo hii. Napenda pia kuwashukuru kwa kuitikia wito wa mkutano na kushiriki pamoja na kuwa na majukumu mengi hasa wakati huu wa mwisho wa wiki. Asanteni sana.

Salamu za Mwaka Mpya

Ndugu Watanzania Wenzangu,

Ninamshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuuona mwaka huu mpya wa 2024. Ninamshukuru sana kwa baraka na mafanikio aliyotujalia mwaka 2023 na ninamuomba baraka na mafanikio zaidi mwaka huu wa 2024.

Kwa ujumla, kwetu sisi hapa Ubalozini, mwaka 2023 ulikuwa ni mwaka mzuri. Nitawaeleza kwa kifupi baadhi ya mambo makubwa tuliyofanikiwa kuyafanya ndani ya mwaka 2023.

Vitambulisho vya NIDA

Mwaka 2023 tumeendelea kushirikiana vizuri na nyinyi viongozi na wanadiaspora mliopo wote hapa Marekani na Mexico. Mathalani, mwezi Januari 2023 kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) tulitoa huduma Vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania wenye sifa katika mpango wa

majaribio (*Pilot Study*). Pamoja na taarifa kuhusu suala hili kutolewa ndani ya muda mfupi, lakini kutokana na ushirikiano wenu, Watanzania walijitokeza na kupata huduma. Tunatarajia kwamba baada ya hatua muhimu kukamilika, vitambulisho hivyo vitaanza kutolewa Ubalozini. Tutawaarifu maamuzi hayo yakifikiwa.

Huduma za Uhamiaji

Mwaka 2023 tuliendelea kutoa huduma za pasipoti; shahada za dharura za *kusafiria (emergency travel documents)*; kushughulikia maombi ya viza; kuhudumia Watanzania walio kwenye changamoto mbalimbali; kuthibitisha, kuidhinisha na kuhakiki nyaraka tofauti; na kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kiuhamiaji.

Tunapozungumzia suala la huduma za uhamiaji, mtakumbuka kwamba tuliahidi kupeleka “Mobile Kit” kwenye majimbo mbalimbali kwa ajili ya kuchukua picha na alama za vidole kwa ajili ya maombi ya pasipoti. Hata hivyo, zoezi hilo halikufanyika kwa mwaka 2023 kama tulivyotarajia kutokana na changamoto mbalimbali. Ubalozi unaangalia uwezekano wa kutoa huduma hiyo mwaka huu wa 2024 na taarifa rasmi zitaletwa kwenu wakati utakapofika.

Ushirikiano kwenye Matukio Mbalimbali

Ndugu Viongozi,

Mwaka 2023 tumeshirikiana kwenye matukio mbalimbali muhimu ikiwemo ya Kitaifa kama maadhimisho ya sikukuu ya Muungano na Siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani. Tulishirikiana pia kwenye shughuli mbalimbali ambazo mliziandaa na kutualika na nyingine ambazo tulizifanya pamoja. Nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu na nawasihi tuendelee kushirikiana mwaka huu 2024.

Uhusiano na Serikali ya Marekani

Ndugu Watanzania Wenzangu,

Kwa upande wa Serikali, mwaka 2023 ulikuwa ni mzuri kwetu pia katika uhusiano wetu na Marekani. Mtakumbuka kwamba mwezi Machi 2023, Mheshimiwa Kamala Harris, Makamu wa Rais wa Marekani alitembelea Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi tatu tu za Afrika alizozitembelea. Ziara hii pia ilikuwa ni ya kwanza ya kiongozi mkubwa wa Marekani barani Afrika tangu mwaka 2015. Ziara hiyo ilikuwa na mafanikio makubwa ikiwemo kutangazwa kwa uwekezaji unaofanywa na kampuni ya Marekani ya Life Zone Metals ambayo inajenga kiwanda cha kuchakata madini mbalimbali adimu (critical minerals) ikiwemo nikeli na kuuza kwenye soko la dunia ikiwemo hapa Marekani ifikapo mwaka 2026.

Vilevile, mwezi Agosti 2023, Wabunge wa Baraza la Wawakilishi (U.S. House of Representatives) wakiongozwa na Mhe. John James, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Afrika iliyo chini ya Kamati ya Mambo ya Nje ya Bunge hilo walitembelea Tanzania.

Viongozi wengine wengi waandamizi wa Serikali ya Marekani waliitembelea Tanzania mwaka 2023. Hii inadhihirisha kuwa uhusiano na ushirikiano baina ya nchi zetu ni mzuri sana.

Uhusiano wetu na Benki ya Dunia na IMF

Ndugu Viongozi wa Jumuiya za Watanzania,

Mwaka 2023 tuliendelea pia kuimarisha uhusiano mzuri uliopo baina ya Tanzania na mashirika ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani (IMF). Uhusiano huo ulipelekea nchi yetu kuendelea kunufaika na fedha za masharti nafuu kutoka kwenye mashirika hayo kwa ajili ya miradi na programu mbalimbali muhimu za maendeleo nchini mwetu.

Utalii

Kwa upande wa sekta ya utalii, hapa Marekani tuliendelea kuongoza kwa kupeleka watalii wengi zaidi nchini Tanzania kwa nchi ambazo ziko nje ya Afrika kwa mwaka 2023. Hapana shaka kwamba filamu ya Tanzania: The Roya Tour ambayo Mheshimiwa Rais alicheza na kuja kuizundua hapa Marekani mwaka 2022 ilichangia sana kwenye mafanikio haya. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Biashara na Uwekezaji

Kwa upande wa biashara na uwekezaji, tuliendelea kufanya vizuri mwaka 2023. Kampuni za Kimarekani ziliendelea kuwekeza nchini katika sekta mbalimbali. Pia, kwa kushirikiana na wadau tofauti tulifanikisha ziara za makundi manne (4) ya wafanyabiashara kutoka hapa Marekani kwenda Tanzania kujionea fursa za biashara na uwekezaji zilizopo.

Aidha, katika jitihada za kuboresha biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Marekani, mwezi Oktoba 2023, tulisaini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) yaliyoanzisha jukwaa la majadiliano ya kibiashara *(U.S.-Tanzania Commercial Dialogue)*. Jukwaa hilo lina lengo la kuboresha mawasiliano ya mara kwa mara kuhusu masuala ya kibiashara ikiwemo kutatua changamoto mbalimbali katika ufanyaji biashara baina ya Tanzania na Marekani. Tunaamini kwamba jukwaa hilo litachangia kwenye kuongeza biashara baina ya Tanzania na Marekani.

Ndugu Viongozi,

Mwaka 2023, mwezi Aprili, Tanzania ilisaini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na Benki iliyo chini ya Serikali ya Marekani inayoshughulikia kuagiza na kuuza nje ya nchi *(Export-Import Bank of the United States – Exim).* Kupitia makubaliano hayo, benki hiyo imetenga kiasi cha Dola za Marekani 500 kwa ajili ya kukopesha kampuni za Marekani zinazotaka kufanya biashara na uwekezaji nchini Tanzania. Hata kampuni za Watanzania waliopo hapa Marekani zinaweza kunufaika na mkopo huu. Mchangamkie fursa hii.

Matarajio yetu mwaka 2024

Ndugu Viongozi wa Jumuiya za Watanzania, kwa mwaka 2024 tunatarajia kuyaendeleza mazuri yote tuliyoyavuna mwaka 2023. Kwa mfano, tunatarajia kukamilisha dhamira yetu ya kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Masuala ya Saratani nchini Tanzania kwa kushirikiana na taasisi iitwayo Global Health Catalyst (GHC) ya hapa Marekani.

Kwa masuala ambayo hatukufanikiwa kama tulivyotarajia kwa mwaka 2023 basi tunachukua kama ni mafunzo ambayo tutayaboresha zaidi baada ya kujifunza. Hivyo, tunahitaji ushirikiano wenu sana mwaka huu 2024 ili tuendelee kufanikiwa na kusonga mbele wote kama Taifa.

Ushirikiano na Diaspora

Ndugu Viongozi,

Katika mwaka wa 2024, Ubalozi utaendelea kuimarisha ushirikiano na Diaspora. Katika hilo, tumejipanga kama ifuatavyo:

- Kukutana na viongozi wa jumuiya za Watanzania angalau mara tatu kwa mwaka. Hapa ninazungumzia kukutana kwa pamoja kama hivi, lakini tutaendelea kukutana mmoja mmoja kadri tunavyotembelea Majimbo mliyomo.
- Kuendelea kushirikiana katika matukio mbalimbali, yale mnayoyaandaa na yale yaliyo katika kalenda ya Ubalozi yakiwemo Maadhimisho ya sherehe za Muungano tarehe 26 Aprili 2024, ambapo tunatimiza miaka 60 sasa na maadhimisho ya siku ya Kiswahili Duniani tarehe 07 Julai 2024 pamoja na shughuli nyingine zitazojitokeza.
- Tunadhamiria pia kuanzisha utaratibu wa kukutana na Diaspora wa Tanzania kwa kuzingatia sekta wanazotoka kwa lengo la kuwatambua, kushirikiana nao na kuwaunganisha na wadau wengine katika kuzifikia fursa zilizopo hapa Marekani

na Tanzania. Kwa kuanza, tutaanza na wataalamu katika sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Nishati, Sekta Binafsi, Tehama na Utalii.

- Ubalozi kuanzisha programu ya kutembelea taasisi za elimu ikiwemo vyuo vikuu vya hapa Marekani kwa lengo la kutambua fursa zinazopatikana katika vyuo hivyo zikiwemo fursa za ufadhili wa masomo na kutengeneza network kwa kushirikiana na Diaspora waliopo katika vyuo hivyo.

Ili kufanikisha haya, tunawasihi kuwaeleza wanachama wenu walio katika fani mbalimbali kujiandikisha hapa ubalozini ili tuweze kushirikiana kwa pamoja kwa maslahi ya Diaspora na nchi yetu kwa ujumla. Tunaomba taarifa hizo zitumwe kupitia barua pepe: diaspora@tanzaniaembassy-us.org.

Suala la Hadhi Maalumu

Ndugu Viongozi,

Katika mkutano wetu wa mwisho nilipata nafasi ya kutoa ufafanuzi wa kina juu ya hatua iliyofikiwa katika mchakato wa kuwapatia Hadhi maalum Diaspora wa Tanzania kama ilivyoahidiwa na Serikali. Nilieleza kuwa kwa sasa mchakato huo upo katika hatua za mwisho kukamilika na kwamba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imewasilisha nyaraka mahususi kuhusu suala hilo kwenye Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kwa hatua zao ikiwemo maamuzi na maelekezo ya vikao vya juu.

Vikao hivyo vimefanyika na kwa sasa suala hili lipo katika hatua za mwisho na tunatarajia kwamba mwaka huu, 2024 hadhi maalumu itaanza kutolewa kwa Diaspora wetu. Hivyo, tunawaomba muendelee kuwa na subira wakati Serikali inakamilisha mchakato huu.

Fursa zinazopatikana Marekani kwa Diaspora

Ndugu Viongozi wa Jumuiya za Watanzania,

Napenda kuendelea kuwakumbusha kuchangamkia fursa za ufadhili, mitaji na mikopo zinazotolewa na taasisi mbalimbali za Serikali ya Marekani kwa maendeleo yenu na maendeleo ya nchi yetu. Baadhi ya taasisi hizo ni *U.S. International Development Finance Corporation (DFC)*, *U.S. Trade and Development Agency (USTDA)* na *U.S. Exim Bank.* Taasisi hizi zinatoa mitaji kwa kampuni zilizosajiliwa hapa Marekani ambazo zinalenga kupeleka huduma au biashara sehemu mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania. Hivyo, kuna fursa ya kutumia kampuni zenu mlizozisajili hapa Marekani kama mnazo au kuanzisha kampuni na kisha kuomba mitaji hiyo na kwenda kuwekeza Tanzania. Vilevile, kuna mashirika kama *U.S. African Development Foundation* (USADF) na Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) ambayo yanatoa fursa za ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Mnaweza kupata fursa zinazotolewa na USAID kupitia tovuti ya: https://workwithusaid.org/.

Ubalozi unaandaa mkutano baina yenu na taasisi hizi ili muweze kufahamu kwa kina namna ya kunufaika na fursa hizi. Tutawasilisha taarifa za mikutano hiyo zitakapokamilika.

Aidha, Ubalozi unawashauri Diaspora wa Tanzania kufuatilia na kuchangamkia fursa inayoletwa na uwepo wa Baraza la Ushauri la Rais wa Marekani kuhusu Diaspora wa Afrika *(President's Advisory Council for African Diaspora Engagement in the United States)*. Baraza hilo lina jukumu la kumshauri Rais wa Marekani na kuandaa programu mbalimbali zinazolenga kuwainua Diaspora wenye asili ya Afrika hapa Marekani na kuimarisha uhusiano baina ya nchi za Afrika na Marekani kupitia kwa diaspora hao. Baraza hilo lilianzishwa kwa amri ya Rais wa Marekani *(Executive Order)* wakati wa Mkutano wa Viongozi wa nchi za Afrika na Marekani *(U.S.-Africa Leaders' Summit)* uliofanyika Desemba 2022. Taarifa zaidi kuhusu Baraza hilo zinapatikana kupitia tovuti ya Ikulu ya Marekani, eneo la *Presidential Actions* za Desemba 2022.

(https://www.whitehouse.gov/briefing-room/presidential-actions/2022/12/13/executive-order-on-establishing-the-presidents-advisory-council-on-african-diaspora-engagement-in-the-united-states/).

Usajili katika Mfumo wa Kidigitali kwa Diaspora wa Tanzania

Ndugu Viongozi,

Kama mnavyofahamu, mwaka jana, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilizindua mfumo wa kidigitali *(one stop shop)* unaosajili taarifa za Diaspora wa Tanzania waliopo nje ya nchi na kuuwanganisha na watoa huduma mbalimbali wa Tanzania, wadau muhimu na fursa tofauti zilizopo nchini kwa urahisi. Mfumo huo unaitwa kwa Kiingereza, Diaspora Digital Hub. Hatua hii ni muhimu katika kuwatambua Diaspora wa Tanzania, kuwasogezea karibu huduma wanazohitaji na kuwashirikisha zaidi katika shughuli mbalimbali za maendeleo ya nchi yetu. Hivyo basi, Changamoto zilizowasilishwa katijka kikao kilichopita zimewasilishwa na zinafanyiwa kazi hivyo napenda kutumia fursa hii kuendelea kuwasisitiza wana diaspora wote wa Tanzania, kupitia nyinyi viongozi kuendelea kujisajili katika mfumo huo unaopatikana kupitia: https://diaspora.foreign.go.tz.

Kuimarisha Jumuiya na taasisi za Diaspora

Ndugu viongozi,

Ubalozi unatambua na kuthamini mchango unaotolewa na makundi mbalimbali ya Diaspora katika sekta za Afya, elimu na ustawi wa jamii. Pamoja na michango hii Ubalozi unaamini bado Diaspora wanaweza kufanya makubwa zaidi iwapo watashirikiana na kukusanya nguvu kwa pamoja. Hivyo tungependa kuona jumuiya zetu, taasisi mbalimbali na hata Diaspora mmoja mmoja kuongeza ushirikiano baina yao kwa maslahi yao na nchi yetu kwa ujumla. Tunatoa wito kwa viongozi wa jumuiya na taasisi zote za Diaspora kuongeza ushirikiano na kufanyakazi kwa pamoja kwa maslahi yenu na nchi yetu kwa ujumla.

Aidha, Ubalozi unaomba viongozi kuimarisha jumuiya zetu kwa kuweka taratibu zitakazowezesha Watanzania wengi zaidi wajiunge na jumuiya hizi tofauti na hali ilivyo sasa ambao wapo Watanzania wengi wapo mbali na jumuiya zetu na wengine kutotambulika hadi pale wanapopata matatizo.

Hitimisho

***Ndugu Viongozi**,*

Katika kuhitimisha hotuba yangu, naomba kuwahakikishia tena kwamba Ubalozi upo kwa ajili ya kuwahudumia na kushirikiana nanyi nyote bila ubaguzi wowote. Vilevile, napenda kuwahakikishia kwamba Serikali yetu chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inathamini mchango mkubwa unaotolewa na Diaspora katika maendeleo ya nchi na kwamba upo tayari kushirikiana na Diaspora katika kustawisha maendeleo yao na nchi kwa ujumla. Ubalozi upo tayari kupokea michango yenu ya mawazo na mnaweza kutuandikia wakati wowote kupitia barua pepe yetu ubalozi@tanzaniaembassy-us.org au kutupigia moja kwa moja kupitia simu za Ubalozi.

Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, nawasihi msisitize kutuunganisha na watu, viongozi, taasisi, kampuni na mashirika yoyote yaliyo kwenye maeneo mliyomo ambayo mnaona yatakuwa na mchango chanya kwenye jitihada zetu za kuleta maendeleo ya nchi yetu na ustawi wa Watanzania. Nyinyi mpo huku muda mrefu, mnajuana na watu wengi, mna uzoefu mkubwa na mmeona mengi. Tunasubiri kuwasikia.

Ninawatakia mafanikio tele na kila la heri kwa mwaka 2024!

Asanteni kwa kunisikiliza. Nawakaribisha kwa michango yenu.

Mungu Ibariki Tanzania! Mungu Ibariki Afrika!